

# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA



## TANGAZO

### **PATA KIWANJA JIJINI DODOMA MAKAO MAKUU YA NCHI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa, Halmashauri imekamilisha upimaji wa Viwanja kwa ajili ya Matumizi mbalimbali ikiwemo Makazi, Biashara, Makazi na Biashara, Taasisi mbalimbali, Sehemu za ibada, na Viwanda na itaviuza kuanzia tarehe 10 Disemba, 2018.

Viwanja vipo katika maeneo ya Mapinduzi 'A', Mtumba, Nala, na Medeli Extension ambayo vina ukubwa wa mita za ujazo tofauti kwa ajili ya matumizi mbalimbali.

Aidha, kwa wale waliochukua viwanja awali katika eneo la Mtumba, Kikombo, na Iyumbu lakini hawajavilipia, viwanja hivyo vitauzwa upya kuanzia tarehe tajwa hapo juu bila wahusika kupewa taarifa yeyote.

Zoezi la uuzaji viwanja litafanyika kuanzia saa 2:00 asubuhi katika eneo la wazi kwenye Ofisi za Jiji zilizopo jirani na Sabasaba (Ofisi Kuu ya Manispaa ya zamani).

Kila anayehitaji kiwanja afike Ofisi za Jiji kwa ajili ya kufanya taratibu kuanzia tarehe tajwa, na atatakiwa kukamilisha malipo yote ndani ya miezi mitatu (yaani siku 90) kuanzia tarehe atakayopewa ankara ya madai.

Tangazo hili limetolewa na:

**Ofisi ya Mkurugenzi  
Halmashauri ya Jiji Dodoma  
10 Disemba, 2018**